THAMANI YA UKWELI YA UMASKINI

na Eleanor Turnbull

Wakati ukimwi hupata mtu mmoja kwa familia basi hufanya maisha ya familia hiyo kubadilika, Mahali mingi hasa Afrika zaidi ya mzazi mmoja huambukizwa ukimwi na hii inamaanisha akiba yote ya familia hutumiwa kuwapeleka hospitali na kununua madawa wanao hitaji na kwasababu wazazi hawa ndio hufanya kazi inamaanisha hawawezi kwenda kazi kwani hawana nguvu za kutosha.
Watoto pia huumia kwani hakuna vyakula vya kutosha nyumbani na pia inabidi waache shule ili waweze kufanya kazi ya nyumbani na pia watoto hawa wanakosa matibabu kwani akiba yote imetumika.Nchi nyigi za Afrika huwa na matibabu ya bure lakini matibab uhaya husaidia wafanyikazi wa serikali na wa makampuni za kibinafsi na wale ambao hawafanyi kazi rasmi na waliokuwa mashambani hawasaidiki, na watu hawa ni zaidi ya asilimia tisini(90%) , kwahivyo inabidi wajitegemee kulipa malipo ya hospitali.

Wakati mwingi ,magonjwa hatari kama ukimwi hausababishi umaskini bali unaeneze umaskini na huleta mzunguko katili kati ya umaskini, magonjwa na vifo ya wazazi.Malipo ya hospitali huongezeka na inabidi familia kuuza mashamba na wanyama.Na hii huwacha familia kuwa na shida mingi , na inabidi jamaa wengine wa familia kutafuta kazi hatari kama vile ukahaba , na hwatumii mipira kwani wanalipwa zaidi. Utafiti uliofanywa mwaka wa inayo itwa 2003 ya **Humans Rights Watch inayo itwa "Policy Paralysis: A Call for Action on HIV/AIDS-Related Human Rights Abuses Against Women and Girls in Africa"** ilionesha mtoto mtot mmoja wa kike akisema yakwamba hangependelea kufanya ukahaba kwani anajua atapata ukimwi na kufa na angependa kufanya ambayo itamsaidia lakini ni ngumu sana kuanzisha kazi.Pia umaskini inawalizimu wanaume kuhama manyumbani na kwenda mjini kutafuta kazi ,kazi hizi kama kuwa madereva na kazi ya kutafuta madini ,kazi hizi ni hatari kwa maisha yao na pia kwasababu ya upweke wanajihusisha na tabia hatari.Na hii huleta umaskini na pia kuharibu mila za jamii.

Kwa miaka tano iliyopita malipo ya matibabu ya ukimwi imepungua na pia kumekuwa na maskizano ya kimataifa kusaisdia nchi zinazoendelea na hii imeongeza upatikanaji wa matibabu ya ukimwi Afrika. Lakini bado inaonekana umaskini na matibabu yasiyotosha inasababisha watu wengi kutumia madawa haya vibaya na hii husababisha matibabu haya kutofanya kazi,watu asilimia 95% hawasaidiwi na matibabu haya kwani miili zao zimezoea. Ingawa nchi mingi Afrika hupeana matibabu ya bure ,bado watu wengi hawatumi madawa haya,

kwani wanapoteza kazi kwasababu kila wakati wanaenda hospitalini,pia nauli ya gari ni ghali,na pia hawana pesa ya kununua chakula na hii huleta mzunguko katili kati ya ugonjwa wa ukimwi na njaa.Lisho isiyotosha husababisha mwili kukosa nguvu na hii husababisha virusi vienee kwa haraka mwilini. Mgonjwa wa ukimwi ambaye haoneshi dalili anahitaji asilimia kumi(10%) ya lisho zaidi ya mtu ambaye hana virusi vya ukimwi na mgonjwa mwenye anaonesha dalili anahitaji aslimia 20 hadi 30 (20%-30%). Nchini Rwanda wagonjwa wengi waliogopa kumeza madawa kwni huongeza njaa na hawana pesa za kutosha za kununua chakula.

Watoto mayatima wanaongezeka kwani wazazi wao wameaga dunia kwasababu ya ukimwi.Wamama wengi waja wazito Afrika wana virusi vya ukimwi , nchini kenya asilimia 16, nchini Zambia asilimia 24 na hii inamaanisha karibu watoto kumi wanazaliwa kila mmoja wao ana virusi vya ukimwi. Kulingana na Utafiti wa UNICEF watoto 15 hadi 20 huambukizwa virusi wakati mama ana mimba, 50 wakati mama ana zaa na asilimia 10 hadi 30 kwa kupitia maziwa ya mama.

National Prevention of Mother-To-Child Treatment (PMTCT) hutumia **Nevirapine** kuteremsha hatari ya mama kuambukiza kwa mwanaye kwa asilimia 40, na dawa hii hutumiwa nchi nyingi Afrika. Njia ya kupata madawa haya yamefanywa rahisi lakini utafiti wa UNAIDS unaonesha huko Malawi ni asilimia tatu tu ya wanawake wajawazito ambao wanahitaji madawa haya, nchi hiyo watoto 30000 wanazaliwa na virusi vya ukimwi.Pia familia mingi ni maskini sana na wanaona haya ya kwenda mahospitalini.

PMTCT hueleza wamama wenye virusi vya ukimwi kuhusu njia zingine za kulisha wanao ili kuteremsha hatari ya watoto wao kupata virusi vya ukimwi kutokana na maziwa ya mama ,lakini nchi mingi Afrika kama vile Ethiopia ambapo hakuna vyakula vya kutosha ni ngumu sana kupata njia nyingine ya kulisha wanao.Pia hata kama kuna maji safi ni ngumu sana kwa familia hizi kununua maziwa ya unga ya kulisha wanao.

Umaskini unaoletwa na ukimwi katka familia mingi maskini Afrika inamaanisha watoto wako katika hatari ya kukosa mahali pa kuishi, kutoenda shule,kukosa matibabu na kukosa chakula.Wakiwa wakubwa watoto hawa huwa katika hatari ya kupata virusi vya ukimwi, kutojua kusoma, kufanya kazi ngumu wakiwa bado watoto na pia kukosa kazi. Pia kitu cha kusitikisha ni kwamba watoto hawa hasa wasichana huwacha shule na kutafuta kazi ili kusaidia familia zao, utafiti unaonesha yakwamba wasichana wengi huaga dunia wakiwa wadogo.Wasichana hawa pia hufanya ukahaba na wazee wanaoitwa ‘sugar-daddies’ na wazee hawa wana wapenzi wengi na wengi wao wana virusi vya ukimwi , watoto mayatima na maskini wanakubali kuishi na wazee hawa kwani wanasaidiwa na pesa na maisha zao kubadilika.

Mwishowe watu wenye virusi vya ukimwi huwa na shida ya pesa na jamaa maisha yao yote, Kutafuta madawa ni ngumu kwani inahitaji pesa na pia wanaogopa kupoteza kazi zao , wagonjwa wa ukimwi wamesema ya kwamba wakiambia marafiki zao kuhusu hali yao wao hudharauliwa.
Pia kutotumia madawa inaweza kusababisha mwili kuzoea madawa haya na mwishowe madawa haya yanawacha kusaidia mwili.
kumaliza uzoeaji wa madawa mwilini inahitaji madawa mengine yenye nguvu ambayo yana hatari zaidi mwilini.Watu wengiAfrika wanaambukizwa ugonjwa wa ukimwi ,utafiti unaonesha milioni25 nukta 8, na hii inamaanisha uchumi wa nchi unaenda chini.
Shida ya nchi hizi za Afrika zinaongezeka kwani bajeti ya mwaka inaongezeka kwani nchi nyingi zinapatia wagonjwa matibabu ya bure. , na hii inamaanisha nchi haziendelei ,barabara hazijengwi na matibabu na masomo ya nchi ni za hali ya chini na hii huteremsha hali ya uchumi ya nchi hizi.Hii shida huongezeka kwani wananchi wengi ambao wamesoma na wangeweza kusaidia nchi hizi kiuchumi huaga dunia na kuwacha watoto pekee yao.na vifo hivi husababisha nchi isiendelee na mzunguko wa umaskini na ukimwi unaendelea.